

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS**

Anwani ya Simu: **"TUME"**
DAR ES SALAAM
Namba ya Simu:0738166703
Fax: 255 - 022 – 246011
Baruapepe:
secretary@psc.go.tz
Tovuti: www.psc.go.tz



TUME YA UTUMISHI WA UMMA,
6 MTA A WA ALBERT LUTHULI,
KITALU NAMBA 10,
S.L.P. 9143,
DAR ES SALAAM.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**TUME YA UTUMISHI WA UMMA IMETOA UAMUZI WA RUF AA 27 NA
MALALAMI KO 6 YA WATUMISHI WA UMMA**

Tume ya Utumishi wa Umma imetoa uamuzi wa rufaa **27** na malalamiko **6** yaliyowasilishwa mbele ya Tume na watumishi wa umma kupinga uamuzi uliotolewa na Mamlaka zao za Nidhamu.


Tume ya Utumishi wa Umma hivi karibuni ilifanya Mkutano wake namba **3** kwa mwaka 2019/2020 Jijini Dar es Salaam. Katika mkutano huo, Tume ilipokea na kutoa uamuzi wa rufaa **27** ambapo kati ya hizo rufaa **21** zilikataliwa, rufaa **1** ilikubaliwa, rufaa **2** zilikubaliwa kwa masharti kwamba zikashughulikiwe upya na Mamlaka zao za Nidhamu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu. Aidha, rufaa **3** zilikataliwa kwa kuwa ziliwasilishwa nje ya muda uliowekwa kwa mujibu wa Sheria.

Kwa upande wa malalamiko, Tume ilipokea na kutoa uamuzi wa malalamiko **6** ambapo kati ya hayo, malalamiko **2** yalikubaliwa, lalamiko **1** lilikataliwa na lalamiko **1** lilikataliwa baada ya kuwasilishwa nje ya muda uliowekwa kisheria. Malalamiko **2** yalikubaliwa kwa masharti ya kuanza upya kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo.

Miongoni mwa makosa yaliyosababisha Watumishi wa Umma kuchukuliwa hatua na Mamlaka zao za Nidhamu ni pamoja na kushindwa kuwasilisha kwa ajili ya uhakiki vyeti vya ufaulu wa elimu ya Kidato cha Nne; uzembe uliokithiri; kuisababishia hasara Serikali; kukiuka maadili na mwenendo mwema wa utumishi wa umma; utoro kazini; kutoa taarifa za uongo kwenye fomu za OPRAS na kushindwa kutekeleza majukumu.

Tume ya Utumishi wa Umma pamoja na majukumu mengine, ina jukumu la kuhakikisha Watumishi wa Umma, Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu wanazingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma wakati wa kutekeleza majukumu yao ya msingi ya kisheria.

Imetolewa na:



Richard M. Cheyo
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
TUME YA UTUMISHI WA UMMA
20 Aprili, 2020